MKULIMA WA
SEVIA

Free copy

JUNI - AGOSTI, 2017 #5

# TANZANIA INAKUHITAJI!

**Nchini Kenya, watu wazima husema matunda ni kwa ajili ya watoto na mboga mboga ni kwa ajili ya sungura. Mboga mboga hazi thaminishwi ipasavyo. Nchini Tanzania pia, mboga mboga hazipewi kipau mbele. Ni wakati wa mabadiliko.**

## Virutubisho muhimu na vitamini





Ukimuuliza mtanzania mwanaume au mwanamke juu ya mlo anao upenda, jibu litakuwa ni ugali na nyama. Au mchuzi wa kuku na baadhi pengine nyanya, vitunguu, pilipili hoho na bamia. Hakuna mtu atakwambia kuwa yeye anapendelea ugali kwa mnavu. Watu sio wazoefu wa kula mboga mboga. Kwa hali hii, Tanzania si ya kipekee. Upendeleo huu unaonekana katika nchi nyingi duniani kote. Migahawa mingi inauza 'burgers', na si mboga mboga.

Hivi karibuni, utafiti uliofanyika Tanzania kuhusu chakula na lishe, ulitoa taarifa yakuwa utapiamlo bado unachangia vifo vya watoto 130 kila siku. Kwa upande mwingine fetma inaongoza kwa kusababisha magonjwa ya moyo na kisukari. Magonjwa haya hugundulika mapema kwa nadra. Mboga zina virutubisho muhimu na vitamini zinazochangia maisha marefu na afya njema. Ni muhimu kwa afya na maendeleo ya ubongo kwa watoto wakati wa ujauzito na kwa watoto hasa miaka miwili ya awali katika maisha yao. Bill Gates anasema kwamba maendeleo haya ya awali yakicheleweshwa hayawezi kufidiwa baadaye. Ni hasara kubwa ya uwezo wa kibinadamu .*

**Angalia video katika mtandao wa Youtube kuhusu neno: Stunted*

## Maboreaha ya www.sevia.biz

Tovuti yetu ni nzuri na tunajivunia kwa hilo. Katika tovuti hii www.sevia.biz utakutana na **majarida yaliyochapishwa, habari kutoka shambani, jumla ya vipeperushi vya SEVIA, miongozo** yetu mipya na pia muhtasari wa **taarifa za utafiti**. Hasa iliyopendekezwa: **moduli ya mafunzo** kwenye mitandao, juu ya usimamizi wa mazao!



Bado kuna haja ya ufahamu wa umuhimu wa mboga mboga katika mlo bora. Utafiti katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga ulionesha kiwango cha juu cha kudumaa, upungufu wa damu na ukosefu wa madini ya chuma. Kwa afya bora kwa kila Mtanzania, tunapaswa kula gramu angalau 200 ya mboga mboga kwa siku. Tuseme sawa na nyanya nne ndogo, karoti nne au mbilingani moja kubwa.

## Haja ya ongezeko la upatikanaji wa mboga mboga

"Ni nini sasa?", Labda unaweza kutuuliza sisi. Unaweza kuendelea na: "Mimi ni mkulima na mimi ninalima mboga mboga." Au: "Mimi ni mtaalamu wa sekta na ninatoa ushauri juu ya namna ya kuongeza uzalishaji wa mboga mboga." SEVIA inakuhamasisha uendelee kufanya hivyo, na kuzalisha hata zaidi, na aina mbalimbali, na bila shaka mboga zenye ubora wa juu. Mahitaji ya mboga yanaongezeka. Hapa Tanzania ongezeko la idadi liko juu na wenyeji wanazidi kuhamia mijini, ambapo hawana namna ya kupata shamba. Maduka makubwa yanahitaji mboga zaidi. Watalii wengi wanatembelea nchi yetu na mahoteli nayo yanahitaji mboga zenye ubora. Katika maeneo mengi ya upatikanaji wa mboga kwa ajili ya lishe bora bado inahusishwa na mbinu duni za uzalishaji, iwe msimu wa kiangazi au masika. Hivyo, kwa mfano, upatikanaji wa mboga mboga masokoni unashuka wakati wa kiangazi, hata vijijini.



*Picha: Richard van Stel*



*Hitaji la mboga zenye ubora linaongezeka*

Je Tanzania inakuhitaji kama mkulima wa mboga mboga? Kuhakikisha mboga nzuri bado zinazalishwa. Wewe ni kiungo muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula! Na SEVIA inaweza kukusaidia kuzalisha mboga wakati wa msimu wowote.

Wakati huo huo tungependa uwe mhamasishaji wa lishe yenye mboga mboga, kwa manufaa ya afya ya Watanzania. Tumia kauli yetu kuwashawishi walio karibu yako ● *(AvS)*

## 'Pakua' miongozo yetu

SEVIA imeandaa miongozo 11, ambapo wakulima wanaweza kupata taarifa watakazohitaji kujua katika kulima mazao bora. Tumeandaa miongozo ya **nyanya chungu/ngogwe, nyanya fupi, bamia, matango, bilinganya, pilipili hoho, pilipili kali, kabichi, karoti, tikiti maji na kitunguu**. Pakua miongozo yetu katika tovuti yetu **www.sevia.biz**! Miongozo yetu pia inapatiakana katika maduka ya pembejeo na pia tunazigawa katika mashamba darasa ya SEVIA. Je! Unataka taarifa zaidi? Uliza wafanyakazi wa SEVIA.



# MBWAMBO KITURURU ni nani?

**Mwezi Aprili 1994, wakati wa kilele cha mauaji ya kimbari nchini Rwanda, Bw Mbwambo Kitururu, Meneja Ugani wa mdau wetu, Tanzania Horticulture Association (TAHA), aligundua wito wake katika kusaidia watu wenye mahitaji kwa kusambaza chakula na kuwapa malazi. "Ndugu zangu walifikiri nilikuwa mwenda wazimu." Hata hivyo aliamua kupanda ndege kutoka Dar es Salaam mpaka Kigali.**

Bw Kitururu alianza safari yake ya huduma kwa kupitia shirika la 'Christian council of Tanzania' ambalo lilikuwa moja ya mashirika machache yaliyokuwa yakitoa huduma kwa waathirika wa vita nchini Rwanda. Pia aliwahudumia wakimbizi wa Rwanda (Kigoma na Kagera). Kwa kupitia Mpango wa Chakula Duniani (World Food Programme - WFP) mwaka 1995, Bw Kitururu alijifunza namna ya kuboresha huduma za misaada Rwanda. Kati ya mwaka 1996 na 2005, alishiriki katika kuanzisha kambi za wakimbizi na kuratibu mipango mbali mbali ya lishe. Akiwa katika shirika la WFP, Bw Kitururu pia alifanya kazi nchini Liberia, Sudan Kusini na Burundi.



## Mpango wa bustani za shule

Katika kipindi hicho, kama mratibu wa mradi, Bw Kitururu alishiriki katika baadhi ya miradi ambayo imesaidia watanzania kuondokana na ukame mwaka 2000. Miradi hiyo ni kama mradi wa mchele wa magugu, miradi mbali mbali ya umwagiliaji na upatikanaji wa masoko. Yeye anajivunia zaidi mpango wa bustani za shule, ambao aliuona katika mmojaya miji aliyo tembelea barani Afrika akitoa huduma. Mradi huu ulitekelezwa katika shule 200 za sekondari za serikali nchini Tanzania, mwaka 2013 -2014. Bw Kitururu alisema:

**Alivutiwa na sekta ya kilimo cha mbomboga na maua kwa sababu aliona matumaini**



"Wakati wa tathmini tuligundua kwamba 80% ya wanafunzi wanaoshiriki katika bustani za shule, pia wameunda bustani nyumbani kwao."

### Kuboresha uzalishaji

Bw Kitururu sasa anafanya kazi na TAHA, akiongoza timu ya maafisa ugani katika mikoa 15 na wakulima 100 katika jamii. Lengo kuu ni kuwafahamisha wakulima wa mbogamboga ngazi mbalimbali za mnyororo wa thamani katika kilimo. Kwa nini Bw Kitururu alivutwa katika sekta hii ya mboga mboga? "Kwa sababu ya sababu rahisi ya kwamba ilionesha matumaini kwa watu wa nchi yangu."



*TAHA wako Zanzibari pia*

Masoko ya matunda na mboga mboga za Tanzania yanazidi kuongezeka, kuanzia na mahitaji ya ndizi nchini Kuwait mpaka viazi vitamu nchini Israeli. TAHA inazidi kutafuta fursa za soko kwa bidhaa za kitanzania na ni wajibu wa Kitururu kuwawezesha wakulima wa mboga mboga kwa kuwapa ujuzi wa kuzalisha mboga mboga zenye ubora kufikia viwango vya kimataifa. TAHA na SEVIA wana hirikiana bega kwa bega katika kutoa elimu kwa wakulima katika uzalishaji bora.

### Kukua kwa sekta ya kilimo cha mbogamboga na maua

Wanasema wema huanzia nyumbani, na Bw Kitururu amehamasika kusaidia kuboresha sekta ya kilimo cha mboga mboga nchini Tanzania kuwa katika kiwango cha kimataifa. Yeye anaamini kwamba katika kipindi cha miaka mitano sekta ya kilimo cha mboga mboga kitachangia angalau 25% ya mapato ya nchi: "Kwa sababu kuna uelewa mkubwa wa fursa za biashara katika sekta ya kilimo, hata miongoni mwa wanasiasa, kwani hata VAT imeondolewa kwenye vifaa kilimo, wakulima sasa wanaweza kutumia vifaa vya kuboresha uzalishaji wao." Bw Kitururu ataendelea kufanya kazi na SEVIA kuhakikisha kuwa wakulima wa mboga mboga, wakubwa kwa wadogo, wanapata msaada wa kiufundi, kwa wote wanao hitaji kuboresha maisha yao. Na falsafa 'mabadiliko huanza na wewe', Bw Kitururu ni mmoja wa mashujaa tunayo bahati ya kuwa nao, kwani wanawezesha mabadiliko katika jamii zetu ● *(CM)*

# KUA MTAALAMU KWA KUJIFUNZA KUPITIA MTANDAO WETU!

**SEVIA imeandaa elimu kwenye mtandao kwa ajili ya wakulima na wataalamu wa kilimo: kuhusu ulinzi wa mazao, kupandikiza na kukuza miche, ratiba za mbolea na virutubisho vya mazao. Elimu hii itaendana na mazingira ya kitanzania na elimu hii inapatikana kwa lugha ya Kiswahili pia. Unaweza kijifunza kwa kutanzama video, ambayo pia inahamasisha. Kuona ni kuamini. Faulu mtihani na utaweza kusimamia karibia kila kitu!**

**Tembelea tovuti yetu www.sevia.biz ambayo tunajivunia kwa sababu tumeshaboresha, hivyo anza mafunzo. Mwishoni mwa mafunzo kuna jaribio la mwisho na baada ya kushinda jaribio hilo utapata cheti.**




# AGENDA

**JUNI**

- Mafunzo kwa wakulima katika kituo cha SEVIA
- Mafunzo kwa wakulima shambani
- Kusimamia shamba darasa
- Mafunzo kwa wataalamu kuhusu uzalishaji katika greenhouse

**JULI**

- Mafunzo kwa wakuima katika kituo cha SEVIA
- Maonesho ya shamba darasa



**AGOSTI**

- Mafunzo kwa wakulima
- Maonesho ya shamba darasa
- Kushiriki katika maonesho ya Nanenane Mikoani Arusha, Morogoro, Dodoma na Mwanza

# TIPS & TRICKS

## Ondoa unyevu katika matawi haraka iwezekanavyo, fahamu magonjwa wakati wa mvua za muda mrefu

**Mvua ni muhimu kwa ustawi wa mazao yako, baada ya mvua majani hufunikwa na unyevu, ambao unaweza kusababisha kuzuka kwa magonjwa ya ukungu, hasa katika mazao ya wazi shambani. Katika makala hii, tutakueleza jinsi ya kuzuia na kudhibiti haya magonjwa ya msimu wa mvua ambayo hujipenyeza katika mazao.**

Baadhi ya magonjwa yanayoathiri mboga wakati wa mvua ni vimelea vya fangasi, magonjwa kama kuoza kiuno, mnyauko bakteria, ubwiri unga, ukungu na barafu na magonjwa ya bakteria kama madoajani na uozo.



*Bakajani chelewa ya nyanya*

### Je, unajua kwamba...

#### Ukaguzi wa mara kwa mara ni muhimu

Wakati wa mvua kagua mazao yako mara kwa mara kwa ajili ya dalili za magonjwa, kwa mfano kila baada ya siku mbili.



*Bakajani katika vitunguu*

Kutambua mapema ni muhimu, kwa sababu kiwango cha maambukizi bado kitakuwa chini hivyo unaweza kuzuia ugonjwa kabla hujaenea. Baada ya kutambua tatizo chukua hatua sahihi kudhibiti ugonjwa huo, kama vile unyunyizaji eneo maalum lililoathiriwa au kuondoa mimea au sehemu za mimea iliyoathiriwa.



#### Kilimo cha ndani kinaweza kupunguza magonjwa

Kupunguza unyevu kwenye matawi ni muhimu ili kupunguza magonjwa. Unaweza kufanikisha hili kwa kupanda mazao chini ya hifadhi au katika wavu au 'greenhouse' . Hizi miundo pia hutoa ulinzi kwa mazao dhidi ya mvua na hali nyingine mbaya kama mvua ya mawe na dhoruba. Mbinu hizi zinahitaji uwekezaji lakini gharam zitalipwa kutokana na mavuno ya juu na gharama za chini dawa.



#### Uchaguzi wa aina na namna ya kukuza miche yenye afya husaidia kudhibiti magonjwa

Mimea yenye afya inaweza kushinda mashambulizi kutoka kwa wadudu na magonjwa. Chagua mbegu zenye uvumilivu au usugu dhidi ya magonjwa na kuza miche yako katika trei au katika kitalu cha ardhi kilicho boreshwa kwa kutumia udongo uliochemshwa. Wakati wa kuanzia na miche yenye afya hauhitaji matumizi mengi ya madawa.

## Matumizi ya boji katika uzalishaji wa mboga mboga inaweza kudhibiti wadudu

Boji hukinga udongo. Boji huzuia vimelea vinavyotokana na udongo kurukia matawi ya mimea. Nyasi au vinginevyo vituiavyo kama boji vinaweza kupunguza magonjwa. Boji ya plastiki ni fanisi zaidi, lakini pia ina gharama kubwa zaidi.



*Matango yenye afya kwa kupitia mbinu za kuinua mimea*

## Kuinua na kushikiza mimea inapunguza kuoza

Kuinua mimea ni muhimu zaidi katika msimu wa mvua kwa matunda ya mboga mboga, kwani matunda huoza kama yakilalala kwenye udongo wenye unyevu kwa muda mrefu, hasa katika nyanya, tango na pilipili. Matumizi ya vigingi na kimia huongeza mzunguko wa hewa uwanjani na kwa sababu kuna mzunguko wa hewa safi magonjwa hupungua. Kuinua mimea pia hupunguza uharibifu wa mazao yako wakati wa kazi. Kwa mfano: Upulizaji wa dawa unaweza kufanyika kwa ufanisi zaidi.



*Bakajani chelewa*

## Zana za kilimo na mashine zinaweza kuwa vyanzo vya maambukizi

Zana za kilimo na mashine hubeba vipande vya mazao, udongo, na maji kutoka shamba moja hadi lingine, hivyo mara nyingi hueneza vimelea au chanzo kingine kinachoanzisha magonjwa. Safisha zana kila wakati baada ya kufanya kazi, kabla ya kwenda kutumia sehemu nyingine ili kupunguza uhamisho wa vimelea na idadi ya wadudu. Ni lazima kusafisha mavazi ya wafanyakazi kabla ya kuhamia shamba lingine.

## Usafi wa mazingira ni muhimu

Msimu wa mvua za masika ni kipindi cha magugu mengi. Huenda tayari yamekwisha ambukizwa ugonjwa, tayari kushambulia mazao yako. Hakikisha shamba lako ni safi wakati wote. Ng'oa mimea yaliyo ambukizwa na kutupa, aidha chimbia au choma mbali na shamba. Ondoa uchafu wote wa mazao baada ya mavuno, kwani vimelea hubaki katika uchafu wa mazao.

## Fahamu magonjwa na kuanza dawa kwa muda

Kulinda mimea yako dhidi ya magonjwa ni muhimu kuanza dawa kwa muda, hivyo ukaguzi mara kwa mara ni muhimu. Kipindi hatari kama kipindi cha mvua za masika, matawi



*Madoa yatokanayo na bacteria*

huongezeka katika mazao, piga dawa ya Mancozeb au Chlorothalonil kila baada ya siku 4-5 pamoja na dawa ya fangasi yenye ufanisi zaidi. Katika kipindi cha jua, ukuaji wa matawi ni wastani, piga Mancozeb tu kila baada ya siku 7-8, itasaidia. Mancozeb ni dawa ya fangas yenye upana mkubdwa. Hulinda mimea dhidi ya aina mbalimbali ya magonjwa na vimelea, lakini unahitaji dawa kabla ya dalili hazija onekana au kusambaa .

Azoxystrobine na Difenoconazole ni dawa nzuri kwa fangasi lakini ni kwa magojwa maalum zaidi na haziwezi kudhibiti magonjwa yote. Kwa hiyo, soma gamba kabla na ujue magonjwa unayohitaji kudhibiti.
Ugonjwa wa mnyauko hauwezi kudhibitiwa kwa kemikali. Hivyo mzunguko wa mazao na usafi wa mazingira lazima dawa ya 'Copper' shaba , lakini ukilinganisha na dawa nyingine za fangasi , 'Copper' haina ufanisi mzuri.

**Wafanyakazi wa SEVIA wanaweza kukusaidia katika hatua zote za usimamizi wa mazao husika. Omba ushauri wetu!**

# HABARI KUTOKA SHAMBANI

**Santateli Sumari ni mkulima wa nyanya kutoka Maroroni B, kwa miaka 20 iliyopita. Wakati anafanya kazi shambani, mke wake Neema husimamia biashara ya duka na mashine ya kusaga hapo kijijini. Siku zote huotesha nyanya kwa kutumia mbegu za kienyeji kutoka katika maduka ya mbegu. Katika kipindi cha masika, hulima ardhi kubwa kama hekta 3 za nyanya lakini kwa kutegemeana na soko, ila faida yake ni ndogo. Hata hivyo, haya yalikua maisha yake kabla ya SEVIA. Toka asimamie shamba darasa la SEVIA shambani kwake mwezi Agosti 2016, sasa anazungumzia mpango wa uzalishaji kwa tumia mbegu bora za mboga mboga kwa ajili ya soko lake.**

"Ilikua mara yangu ya kwanza kutumia mbegu chotara, nmetumia Jarrah F1 na Kipato F1 kwa nyanya na kwa mara yangu ya kwanza kuzalisha matango ambapo, nilitumia mbegu aina ya Monalisa", alisema bwana Sumari. "Katika miaka yangu yote ya kilimo, sikuwahi kuhesabu mbegu kwa usahihi na nafasi kati ya mmea na mmea, nilipenda kuweka miche karibu ili kuokoa nafasi kwa matumaini ya kupata





mavuno mengi. Sikujua kwamba msongamano unaleta mazingira yasio ya afya kwa mmea, na kupelekea kukabiliwa na magonjwa. Hii ilinigharimu fedha nyingi."
Wakati wa akijifunza na Iddi Haridi (afisa ugani wa SEVIA) kama mkulima mwenyeji, alipata mafunzo ya namna sahihi ya kuhesabu mbegu, maandalizi ya shamba na vipimo vya madawa. "Nilikua natumia TZS 50,000 kwenye madawa kwa wiki katika heka moja' Alisema, "lakini sasa nimetumia shilingi 50,000 Na nimetengeneza faida ya shilingi 400,000 kwa kuuza matango. SEVIA ilinifundisha jinsi ya kutengeneza faida."

## *SEVIA inatufundisha kufaidika*

Bwana Sumari kwa sasa analima ½ (nusu) heka badala ya heka 3, na anatumia pia nafasi iliyopendekezwa kati ya mmea na mmea inayomsaidia kusimamia mazao kwa urahisi. Amepanga kuweka dripu kwa ajili ya umwagiliaji kwa shamba lake la nje na baadae kujenga 'greenhouse'. Wakati mwingine, kidogo ni kingi ●" *(CM)*

# WATU @ SEVIA

## Ukuaji katika huduma ya ugani!

**SEVIA inatambua umuhimu wa kufikia wakulima mboga mboga na kufundisha maarifa sahihi. Ndiyo maana tuko radhi kukua na kutoa huduma ya ugani katika wilaya ya Kondoa, Njombe, Manispaa ya Mbeya na wilaya ya Misungwi. Mbali na hilo, mkufunzi Mary Maganga ameajiriwa kuwezesha mafunzo yote yatakayofanyika katika kituo cha SEVIA. Amini tuko kwa ajili yako!**



*Kutoka kushoto hadi kulia: Mary Maganga, Wilfred Makange, Franco Frederick, Mseti Mwita, Athumani Issah and Andrew Nyambega*

# Mahanjumati Namna ya kuandaa Brokoli

### Mahitaji

- *Kichwa cha Brokoli 1*
- *Kitunguu kilichokatwa 1*
- *Kitunguu Swaumu ½ kijiko cha chai*
- *Mafuta ya kupikia au siagi kijiko 1*
- *Chumvi na pilipili manga*
- *Uamuzi: maharage mabichi na caroti (vikatwe kwa marefu na nyembamba kiasi, na kuchemshwa kwa kiasi)*



### Njia

Chemsha maji kwa muda wa dakika 5-10. Safisha kisha kata vitawi vya mboga (usitumie shina wala majani yake) katika saizi ndogo au ya kati, na kuweka katika maji ya moto (yakiyo kwisha chemka). Basi chemsha kwa dakika 5-7 ilimradi isivie sana. Ondoa kwenye jiko na kuchuja maji . Weka sufuria nyingine jikoni na kisha weka mafuta ya kupikia. Kaanga vitunguu na vitunguu swaumu kisha ongeza brokoli (pamoja na maharage mabichi na karoti ulizoweka kando). Kaanga mboga kwa muda wa dakika 3-5, ongeza chumvi na pilipili kuleta ladha. Pakua wakati ya moto, inafaa kwa ugali, tambi au wali!


MKULIMA WA SEVIA

Wachangiaji

SEVIA, P.O. Box 7211, Moshi

**Anuani ya kutembelea**
Lambo, Mferejini
Tanzania
+255 685 942 364
www.sevia.biz

**Michango ya jarida hili ni kutoka kwa**
- Anita van Stel
- Clara Mlozi
- Elijah Mwashayenyi
- Epaphras Milambwe
- Herman de Putter
- Mary Maganga

**Wahariri**
Clara Mlozi
Anita van Stel

**Ubunifu**
Mooizo Design

• Wageningen UR • SEVIA • Communications consultant


**Je, unataka kupokea nakala za bure za awali za jarida hili? Tafadhali tuma barua pepe au soma jarida katika tovuti yetu www.sevia.biz**